NATnets news

Toleo Na. 11

Oktoba - Disemba 2009

## Mzunguko wa 8 wa Mfuko wa Fedha Wawezesha Kampeni ya Upatikanaji Vyandarua kwa Wote

Mnamo tarehe 2 Oktoba, 2009, Mzunguko wa 8 wa Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria ulitiwa saini rasmi mjini Geneva, Uswisi.

Mfuko huu utafadhili kampeni ya kwanza ya Tanzania ya Usambazaji wa Vyandarua kwenye sehemu za malazi ambayo itatilia mkazo katika usambazaji wa Vyandarua vyenye Dawa ya Kudumu kwenye kaya kupitia mikakati mbalimbali ili kufanikisha upatikanaji wa Vyandarua vyenye Dawa ya Kudumu kwa watu wote, kuimarisha miundombinu ya malaria katika ngazi ya mkoa na kuweka msingi wa kuainisha taratibu za maendeleo endelevu ya upatikanaji wa huduma kwa wote katika siku za baadaye.

Kampeni hii inatarajiwa kuanza ifikapo robo ya kwanza ya mwaka 2010 na itatekelezwa kwa miezi saba. Wakati wa utekelezaji, inatarajiwa kuwa Vyandarua zaidi ya milioni 14.6 vitasambazwa, hivyo kuwezesha upatikanaji wa vyandarua viwili kwa kila kaya. Hadi kufikia mwishoni mwa kampeni hii, Tanzania inatarajia kuvuka lengo la kufikia asilimia 80 ya upatikanaji wa vyandarua kwa nchi nzima, hii ikiambatana na kushuka kwa maambukizo na vifo vinavyotokana na malaria.

Mfuko wa Fedha wa Dunia ulianzishwa mwaka 2001 kama ubia baina ya sekta ya umma na binafsi kuzisaidia nchi zinazoendelea kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.

## Ndani ya Toleo Hili:

**Ukurasa wa 2**
- Tahariri
- Utafiti wa Vyandarua Wasaidia Jitihada za Kupambana na Malaria

**Ukurasa wa 3**
- Maendeleo ya Tanzania katika kufikia malengo ya Abuja

**Ukurasa wa 4**
- Wizara ya Afya yatoa Mafunzo kwa Wanahabari
- Dk. Mwita adokeza kuhusu kampeni ya vyandarua kwa wote

# NMCP Yazindua Hati Punguzo Mpya

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP) imezindua Hati Punguzo Mpya zitakazotolewa kupitia kampeni ya *Keep Up*. Hati punguzo mpya itatatua changamoto za bei na usawa katika upatikanaji wa vyandarua. Hadi kufikia Desemba 2009, wajawazito na watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja wataweza kununua vyandarua vyenye dawa ya kudumu kwa shilling 500/- tu.

**(Inaendelea Uk. 2)**



*Bw. Misheck Ndaskoi akiatoa chandarua chenye dawa ya kudumu kwa mlengwa wakati wa uzinduzi wa Hati Punguzo mpya.*

## Zaidi ya Vyandarua Milioni 4.9 Vyawanufaisha Walengwa

Hadi kufikia mwezi Septemba 2009, Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo umeweza kusambaza zaidi ya Vyandarua Vyenye Dawa milioni 4.9 kupitia sekta binafsi. Hii ina maana kwamba zaidi ya watoto wachanga milioni 1.1 na wanawake wajawazito milioni 3.7 wananufaika kupitia mpango huu.

Inatarajiwa kuwa wajawazito na watoto wengi watanufaika kwa kiasi kikubwa na utaratibu mpya wa Hati Punguzo ya bei nafuu zaidi, ambapo watatakiwa kuongeza Tsh. 500 tu kununua vyandarua. Hati Punguzo iliyoboreshwa itaanza kutumika mwishoni mwa mwaka 2009.




Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria

# Tahariri

Karibu katika toleo la 11 la "NatNets News". Tunapokaribia mwaka 2010, toleo hili linakuletea mikakati iliyopita, ya sasa na mipango ya baadaye inayotegemewa kuharakisha mafanikio ya kufikia Malengo ya Abuja 2010 ya Upatikanaji wa Vyandarua vyenye Dawa.

Tunamaliza mwaka kwa habari za kusisimua juu ya kutiwa saini kwa Mzunguko wa 8 wa Mfuko wa Fedha wa Dunia ambao unatarajiwa kufadhili "Kampeni ya Upatikanaji wa Vyandarua kwa Wote" ambayo itajikita katika usambazaji wa Vyandarua Vyenye Dawa ya Kudumu milioni 14.6 kwa jamii nzima, na hivyo kuileta Tanzania karibu zaidi ya kufikia lengo la kitaifa la upatikanaji wa Vyandarua Vyenye Dawa vya Kudumu kwa asilimia 80.

Pia tunatafakari mafanikio ambayo Tanzania imeyapata katika kufikia malengo ya Abuja ya upatikanaji wa Vyandarua Vyenye Dawa. Katika makala hii tunaangalia kwa ujumla matukio muhimu katika upatikanaji wa Vyandarua vyenye Dawa kwa walengwa, matarajio yanayotegemewa na baadhi ya mambo muhimu yaliyoleta mafanikio.

Tunayo furaha kuwaletea makala kutoka kwenye uzinduzi wa Hati Punguzo mpya itakayowawezesha wajawazito na watoto kununua vyandarua vyenye dawa kwa shilliingi 500/- tu. Mwisho tunawaletea habari kutoka kwenye warsha ya mafunzo iliyotolewa na Wizara ya Afya kwa waandishi wa habari.

Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa wale wote waliotutumia michango yao kwa toleo hili. Ni matumaini yetu kwamba kuendelea kwako kuunga mkono jarida kutabaki kuwa njia muhimu ya kuchangia shughuli na mafanikio ya NatNets.

Uchapaji na usambazaji wa toleo hili umefadhiliwa na Swiss Tropical institute ambaye ni Wakala Mkuu wa SDC chini ya kitengo kinachoratibu maswala ya vyandarua vyenye dawa (ITN Cell).

**NATnets News imetolewa na**
ITN Cell
Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria
S. L. P. 3430
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2124 977
Nukushi: +255 22 2124 976
Barua-pepe: info@natnets.org

**Imeandaliwa na**
MediaNet Limited
S. L. P. 8608
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2760 288
Barua-pepe: info@medianettz.com

# NMCP Yazindua Hati Punguzo Mpya

*(Inatoka Uk. 1)*

Wakati wa uzinduzi, Mgeni rasmi – Bwana Misheck Ndaskoi – Mkurugenzi katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto alikiri kuwa serikali imechukua hatua mbalimbali muhimu kuzikinga familia na ugonjwa wa malaria, ikiwa ni pamoja na utoaji wa vyandarua vyenye dawa kwa bei nafuu. Aliwasisitiza wajawazito kuhudhuria Kliniki za Afya ya Mama na Mtoto mapema zaidi wakati wa ujauzito ili waweze kupata Hati Punguzo itakayowawezesha kununua vyandarua vyenye dawa ili kujikinga na mbu waenezao malaria. Aliongeza kuwa, shughuli za pamoja za kupambana na malaria kwa kutumia vyandarua vyenye dawa, ugunduzi na matibabu ya mapema ya malaria, na matumizi ya dawa mseto zitaisaidia nchi kupunguza vifo vya kina mama na watoto vinavyotokana na malaria.

Akiongea kwa niaba ya Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Dk. Geoffrey Kiangi – alisema kuwa serikali itatoa vyandarua vyenye dawa kuwafikia wajawazito na watoto wote wenye umri chini ya umri wa mwaka mmoja Tanzania Bara. Pamoja na hayo, alitilia mkazo kuwa serikali na wadau wake haitavumilia wauzaji wanaopandisha bei za vyandarua zaidi ya shilling 500.

Tofauti na jitihada nyingine, Mkakati wa *Keep Up* utawawezesha walengwa kuchagua aina yoyote ya chandarua wanachopendelea, hii itasaidia kuondoa changamoto za kiutamaduni na kidini zinazozuia matumizi ya vyandarua. Kampeni hii inategemewa kutekelezwa pamoja na kampeni ya usambazaji vyandarua kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano inayotegemea kumalizika mnamo mwezi Machi 2010. Kampeni zote zitafuatwa na Kampeni ya Usambazaji Vyandarua kwa Wote inayolenga kutoa vyandarua kwa kila sehemu ya malazi katika kaya.

Kampeni hii inatekelezwa na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kwa kushirikiana na Mennonite Economic Development Associates (MEDA), World Vision Tanzania, Population Services International (PSI), and A to Z textile manufacturers Ltd. Mipango yote inafadhiliwa kwa ushirikiano baina ya Mfuko wa Fedha wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria, Benki ya Dunia na Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani.

*Dk. Geoffrey Kiangi – alisema kuwa, serikali itatoa vyandarua vyenye dawa kuwafikia wajawazito wote na watoto wote wenye umri chini ya umri wa mwaka mmoja Tanzania Bara*

# Utafiti wa Vyandarua Vyenye Dawa Wasaidia Jitihada za Kupambana na Malaria

Warsha ya kisayansi iliyoandaliwa kwa pamoja na Swiss Tropical Institute (STI) na Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ilifafanua umuhimu na mchango wa utafiti wa Vyandarua Vyenye Dawa katika kudhibiti malaria Tanzania.

Utafiti wa Vyandarua Vyenye Dawa ulijaribiwa kwa mara ya kwanza wilayani Kilombero miaka ya 90 kupitia Mradi wa Kilombero Nets (KINET) uliofadhiliwa na STI na kutekelezwa na Ifakara Health Institute (IHI). Kupitia mradi huu, jina kuu la vyandarua vyenye dawa lilianzishwa na kutangazwa kwenye jamii kupitia uhamasishaji wa jamii.

Uzoefu na mafunzo ya mradi wa KINET unaonyesha kuwa, utafiti wa vyandarua vyenye dawa na kuendeleza matumizi ya vyandarua kupitia mpango wa hati punguzo unachangia kwa kiasi kikubwa katika kuamsha mahitaji, kuwafikia walengwa na kuendeleza matumizi ya vyandarua vyenye dawa vinavyosaidia kupunguza ueneaji wa malaria na hatimaye kupunguza malaria na vifo vitokanavyo na malaria kwa watoto na wajawazito.

Uzoefu wa mradi wa KINET umewezesha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupanga na kutekeleza kikamilifu Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo (TNVS) unaosimamia utoaji wa hati punguzo zinazotumila kununua vyandarua vyenye dawa kwa wajawazito na watoto.

Uswizi, kupitia Swiss Tropical Institute, ina historia ya muda mrefu ya kufadhili utafiti wa malaria nchini, hasa matumizi ya vyandarua vyenye dawa. Katika kuonyesha ushirikiano zaidi kwenye jitihada za kupambana na malaria, Balozi wa Uswisi nchini, Mhe. Adrian Schlaepfer, alitoa ahadi ya dola za kimarekani million moja zitakazotumika kuziba pengo la upatikanaji wa vyandarua kwenye kampeni ya usambazaji vyandarua kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

## Kutimiza Ahadi: Maendeleo ya Tanzania katika kufikia Malengo ya Abuja ya Upatikanaji wa Vyandarua Vyenye Dawa

Wakati wa Mkutano wa Afrika wa "Tokomeza Malaria" uliofanyika jijini Abuja mnamo mwezi Aprili 2000, Viongozi wa serikali na nchi za Afrika waliazimia kwamba angalau asilimia 60 ya wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano wakingwe na malaria kupitia matumizi ya Vyandarua vyenye Dawa.

Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo ni mwitikio wa mkakati wa Tanzania katika kutimiza azimio hili. Mpango huu ulianzishwa mwaka 2004 na unawawezesha wajawazito na watoto wanaohudhuria kliniki za afya ya mama na mtoto kwa mara ya kwanza kupata Hati Punguzo ambayo inaweza kutumika kununulia Chandarua chenye Dawa.

Kwa karibu miaka mitano tangu kuanzishwa kwake, mpango huu umetekelezwa sanjari na jitihada mbalimbali zilizolenga kubadili tabia kupitia kampeni za kukuza matumizi, Vyandarua vyenye Dawa na kujenga mfumo wa kibiashara wa usambazaji wa vyandarua.

### Kuendeleza Soko la Vyandarua Vyenye Dawa

Hadi kufikia Juni 2009, mpango wa Hati Punguzo umeweza kuwafikia wajawazito na watoto zaidi ya milioni 4.9 na kuwapatia Vyandarua Vyenye Dawa.

Mafanikio ya mpango yalianza kwa kuanzishwa kwa Mpango wa Kijamii wa Ukuzaji wa Soko la Kibiashara la Vyandarua vyenye Dawa Tanzania (SMARTNET) (ambao ulijulikana kama SMITN) mnamo Julai 2002 kama chombo cha kijamii cha kukuza masoko ambacho kilikuwa na jukumu la kuhamasisha ubia baina ya sekta ya umma na binafsi, kupanua soko la kibiashara la Vyandarua Vyenye Dawa na kuhamasisha mahitaji na utumiaji wa Vyandarua Vyenye Dawa.

Ripoti ya Sensa ya Maduka ya Rejareja ya mwaka 2007–08 inaonesha kuwa idadi ya maduka yanayouza Vyandarua Vyenye Dawa imeongezeka kutoka 2,282 mwaka 2004/5, 2,364 mwaka 2006/7 na kufikia 6,912 mwaka 2008. Hii inaonesha ongezeko la maduka takribani 973 kati ya mwaka 2007 na 2008.

Upatikanaji wa Vyandarua Vyenye Dawa umeongezeka sehemu nyingi ambapo kuna angalau kliniki moja ya afya ya mama na mtoto inayotoa Hati Punguzo kwa wajawazito na watoto katika kila kata, na hii imehamasisha kuwepo kwa angalau duka moja katika kata linalouza Vyandarua Vyenye Dawa na kupokea Hati Punguzo.



*Duka la rejareja la kuuza vyandarua vyenye dawa Lushoto*

### Kushugulikia Masuala ya Usawa

Ili kuyafikia makundi yaliyoko hatarini zaidi, mipango miwili ya Hati Punguzo ilianzishwa mwaka 2004 na 2006, hizi ni Hati Punguzo ya Wajawazito na Hati Punguzo ya Watoto. Hadi kufikia Septemba 2009, Hati Punguzo za Wajazito zipatazo 3,754,538 na Hati Punguzo za Watoto 1,193,684 zilitumika kununua Vyandarua Vyenye Dawa.



*Mama mjamzito akipokea Hati Punguzo wakati anapotembelea kliniki ya afya ya mama na mtoto*

### Kuyafikia Makundi Yaliyo Hatarini

Ili kuhakikisha makundi yote yaliyo hatarini yanalindwa dhidi ya malaria, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali unatekeleza kampeni ya usambazaji wa Vyandarua Vyenye Dawa ya Kudumu kwa muda mrefu kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano.

Kupitia kampeni hii Vyandarua vyenye dawa vya kudumu vipatavyo 5,564,624 vimesambazwa kwa watoto katika mikoa 13 ya Tanzania bara.Mikoa mingine 8 iliyobaki itafikiwa Machi 2010. Kampeni hii inakusudia kuongeza umiliki na upatikanaji wa vyandarua kwa watoto chini ya miaka mitano kutoka asilimia 25 (2008) hadi kufikia asilimia 80 (2010).

Hadi Septemba mwaka huu, zaidi ya vyandarua 500,000 viliwekwa viuatilifu hivyo kuongeza kinga kwa jamii nzima katika mikoa husika.

### Kushughulikia Jinsi ya Kumudu Gharama

Ili kuongeza upatikanaji wa muda mrefu wa Vyandarua Vyenye Dawa kupitia mpango wa Hati Punguzo, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria umezindua Hati Punguzo mpya mwezi Oktoba 2009 yenye bei nafuu zaidi kwa lengo la kushughulikia changamoto za bei. Mpango huu mpya wa Hati punguzo unawawezesha wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja kununua vyandarua vyenye dawa ya kudumu kwa kuongeza Tshs. 500 tu.

### Kufikisha Kinga kwenye Kaya

Kinga dhidi ya malaria kwa kaya nzima itafikishwa kupitia utekelezaji wa "Kampeni ya Upatikanaji wa Vyandarua kwa Wote" inayotarajiwa kuanza katika robo ya kwanza ya mwaka 2010. Kampeni itaweka mkazo katika usambazaji wa Vyandarua vyenye Dawa kwa wananchi kwa ujumla na hivyo kufikia walengwa wasiofikiwa na mpango wa Hati Punguzo na kampeni nyinginezo.

Inatarajiwa kwamba Vyandarua milioni 14.6 vitasambazwa katika kila kaya. Kampeni itakapokamilika, Tanzania inatarajia kufikia lengo la kufikisha kinga kwa asilimia 80 ya upatikanaji wa Vyandarua vyenye Dawa vya Kudumu kwa nchi nzima.

### Mafanikio Yetu

- Baadhi ya mafanikio yetu kuelekea kufikia malengo ya Abuja ya upatikanaji wa Vyandarua Vyenye Dawa ni pamoja na:
- Hadi kufikia Septemba 2009, zaidi ya Hati Punguzo milioni 4.9 zimetumika kununua vyandarua vyenye dawa na wajawazito na watoto
- Vyandarua Vyenye Dawa vya Kudumu vipatavyo 5,564,624 vilisambazwa kwa watoto chini ya miaka mitano, kupitia kampeni ya usambazaji wa vyandarua.
- Hadi mwaka 2008, maduka 6,912 ya rejareja yanashiriki katika mpango wa Hati Punguzo.
- Kila kata ina angalau kliniki moja ya wajawazito inayotoa Hati Punguzo na duka moja linalopokea Hati Punguzo kwa kubadilishana na Vyandarua Vyenye Dawa.

### Mafanikio yanayotarajiwa

- Hati Punguzo zipatazo milioni 3.2 zinatarajiwa kutolewa chini ya mkakati wa punguzo la bei na hivyo kuwanufaisha watoto na wajawazito kwa miaka miwili ijayo.
- Vyandarua Vyenye Dawa vya Kudumu milioni 14.6 vinatarajiwa kusambazwa katika kaya kupitia Kampeni ya Upatikanaji wa Huduma Vyandarua kwa wote na hivyo kufikia lengo la upatikanaji wa Vyandarua Vyenye Dawa vya Kudumu kwa asilimia 80 nchi nzima.

### Vipengele vya Mafanikio

- Baadhi ya mambo makuu yaliyoleta mafanikio upatikanaji wa Vyandarua Vyenye Dawa ni pamoja na
- Makundi ya walengwa yaliyoainishwa vyema, hususani wale walio hataritni zaidi na malaria.
- Mawasiliano ya kimkakati yaliyobuniwa kuhamasisha mahitaji na matumizi.
- Mfumo rahisi na fanisi wa utoaji huduma na bidhaa kupitia Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi.
- Kujenga ubia na mashirika sahihi ili kutekeleza mikakati mbalimbali.

# Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Yatoa Mafunzo kwa Waandishi wa Habari

Mnamo Septemba 2009, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP) iliendesha warsha ya mafunzo kwa waandishi wa habari. Warsha ililenga kuwapatia waandishi wa habari taarifa za mikakati mbalimbali ya kudhibiti malaria kwa madhumuni ya kujenga uelewa mzuri, kufahamu athari za malaria kwenye jamii na kuwahimiza kuandika makala juu ya madhara ya ugonjwa huu ili kuamsha ufahamu.

Warsha hii ilibuniwa kujenga uelewa mzuri zaidi wa mchango wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC) kupitia wakala wake, Swiss Tropical Institute (STI) katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Vyandarua vyenye Dawa (NATNETS). Warsha hii pia ilifadhiliwa na Mfuko wa Rais wa Marekani (PMI) na STI.

Takribani waandishi wa habari na wahariri 70 kutoka vyombo mbalimbali vya habari vya walielimishwa kuhusu mikakati mbalimbali ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria ikiwemo Kampeni ya usambazaji vyandarua kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano, Mkakati ya kuendeleza matumizi ya vyandarua, na Kampeni ya Upatikanaji wa huduma za afya kwa wote. Mikakati mingine muhimu kama vile Kupuliza Viuatilifu Ndani ya Nyumba, Matibababu Maalum ya Malaria kwa Ujauzito (IpTp), na Utambuzi wa Mapema wa Malaria na matumizi ya dawa ya Mseto pia yalijadiliwa.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, iliyosomwa kwa niaba yake na Dk. Peter Mmbuji, Dk. Donan Mmbando (Mkurugenzi wa Huduma za Kinga) aliwaelezea waandishi wa habari kuwa ni wabia wenye ushawishi mkubwa katika kuwasiliana na kuelimisha wana-jamii juu ya njia sahihi za kujikinga na kuzuia malaria.



*Baadhi ya waandishi wa habari na wahariri wakijadiliana kwenye makundi wakati wa mafunzo juu ya Malaria*

Aliwasihi wana habari kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Afya katika juhudi zake za kusambaza habari ili kuongeza maarifa na uelewa wa umma juu ya njia za kukinga na mbinu sahihi za kutibu malaria.

Kwa upande wao, waandishi wa habari walipendekeza kuanzishwa kwa mtandao ambao utakutana mara kwa mara kupata taarifa mpya juu ya malaria nchini Tanzania na kusambaza habari muhimu kwa umma. Walieleza kwamba utoaji wa habari zinazohitajika na za kutosha mara kwa mara zitaufanya umma uwe na uelewa zaidi na hivyo kuwahamasisha kutafuta njia zinazofaa za kinga na matibabu dhidi ya ugonjwa huu.

# Dk. Mwita adokeza kuhusu Kampeni ya Vyandarua wa Wote

Mnano Oktoba 2, 2009, Mzunguko wa 8 wa Mfuko wa Fedha wa Dunia ulitiwa saini rasmi mjini Geneva, Uswisi. Kupitia ruzuku hii, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itatekeleza kampeni ya kwanza ya "Usambazaji wa Vyandarua kwa Wote".



*Dk. Alex Mwita, MNCP*

NatNets news iliongea na Dk. Alex Mwita, Meneja wa Mpango wa Kudhibiti Malaria kuhusu kampeni hii.

## Swali na Jibu

**S. Nini kiliwasukuma kutuma maombi ya kutekeleza Kampeni ua Usambazaji wa Vyandarua?**
Ili kuona mabadiliko makubwa zaidi, kuna haja na kupanua matumizi ya vyandarua. Hivyo basi ni lazima kuifikia jamii nzima ili kuona matokeo chanya. Hatuwezi kutokomeza malaria bila kuongeza matumizi ya vyandarua.

**S. Je ni mikakati ipi imepangwa baada ya kampeni hii?**
Tutaendelea kuhakikisha upatikanaji wa vyandarua, hii itasaidia uendelevu wa matokeo kwa miaka mingi ijayo na hivyo basi kupunguza maambukizo ya malaria kwenye jamii.

**S. Je NMCP itahakikisha vipi wamiliki wanaendelea kutumia vyandarua?**
Tutaendelea kutoa elimu na majadiliano na jamii ili kuendeleza tabia ya kulala kwenye chandarua kila siku. Vilevile, tunaendelea kuhamasisha jamii ili kuhakikisha kuwa kuna mahitaji na matumizi ya vyandarua. Pia elimu ya mara kwa mara, pamoja na zoezi la kupita Nyumba kwa Nyumba kutoa elimu litaimarishwa.

**S. Jitihada gani zimewekwa kudhibiti matumizi mabaya ya vyandarua?**
NMCP inatambua kuwa kuna baadhi ya wanajamii wanatumia vyandarua kwa kuvua samaki. Hata hivyo, changamoto hii inatokea mara chache sana. Kukabiliana nayo, NMCP inatoa taarifa na elimu juu ya matumizi sahihi ya vyandarua na faida za kiafya zinazotokana na matumizi hayo.

Wadau wetu

Wahisani wetu